MATUMAINI PROG NO:2386
TITLE: WHO WILL GO TO HEAVEN?

SUMMERY: KINAANGAZIA KUHUSU ATAKAYE UONA UFALME WA MBINGUNI.

TEXT: WAEFESO 5:1-7

MADA: NANI ATAKAYE INGIA MBINGUNI?

……

Nakusalimu tena popote ulipo mpendwa nikiwa tena nachukua nafasi hii katika kukukaribisha kwenye somo la leo kwa sababu ya kujifunza kutoka kwenye Neno lake ambalo ni Bibilia.

Hii ni kwa sababu ya upendo Wake kwetu sote.

Nakukaribisha katika kipindi hiki cha Matumaini kutoka TWR Nairobi.

U hali gani? Natumai ya kwamba, tangu wakati wa Mwisho kupatana nawe, ungali mzima katika Bwana.

Kwenye kipindi hiki cha Leo tunaanza kuangazia ujumbe kutoka kwenye Waraka wa Mtume Paulo kwa Waefeso Sura yake ya Tano kuanzia aya ya kwanza hadi ya saba.

(Waefeso 5:1-7)

Kutokana na waraka huu,,,tunapata swali hili ya kwamba,,,,Je1 ni nani atayeingia Mbinguni? Kwa kulimalizia somo la leo,,,nitakuwa nashiriki nawe anwani yangu ili tukaweze kuzungumza kwa ajili ya kusaidiana.

Naitwa Vincent Amara. Nawakaribisha kwanza kabisa watumishi Papi Clever,Dorcas ft Merci Pianist na wimbo,,,E′Mungu mwenye Nguvu.
……..

WIMBO:.....

Ni watumishi Papi Clever,Dorcas ft Merci Pianist na wimbo,,,E′Mungu mwenye Nguvu.
……..

OMBI.Mungu wetu Mkuu Uliyetukuka tena kuliko vyote,,, ni wakati mwingine tunapokuja mbele Zako kwa kunynyekea na ombi ya kwamba,,,ukaweze kutufunilia leo kuhusu yule ambaye ataingia Mbinguni kuwa pamoja Nawe .Tuongoze katika somo hili la leo..ni kwa Yesu Kristo tumeomba… ----Amen

Karibu tena katika kipindi hiki cha Matumaini kutoka TWR jijini Nairobi. Leo hapa kunalo swali ya kwamba,,,Je!,,,ni nani atakaye ingia Mbinguni?

Ujumbe ni kutoka kwenye Waraka kwa Waefeso 5:1-7

Msikilizaji,,kama sisi Wakristo tujuavyo ni kwamba,,,kunayo maisha baada kifo maana maisha ya hapa duniani ni mafupi mno.

Maisha yetu ya humu ulimwenguni huanza punde tu mtu anapozaliwa.

Tuapo yasoma maandiko,,tunaambiwa ya kwamba,,maishakamwe hayana mwisho.

Kama kila mmoja wetu ajuavyo ni kwamba,,,maisha hapa duniani yataisha lakini kuna maisha baada ya hapa ulimwenguni.

Dada yangu,,wasiwasi wetu mkubwa zaidi unapaswa kuwa kwa saababu ya kujiandaa sasa kwa maisha hayo.

Biblia inatufundisha kwamba maasha baada ya ulimwengu huu yatakuwa yenye adhabu kwa wale wanao tenda maovu,,,yaani wale ambao ni wafuasi wa muovu Shetani.

Rafiki yangu,,wewe pamoja nami ambao ni wafuasi wa Kristo,,,bila shaka tutafurahi pamoja Naye katika maisha ya milele.

Maisha yetu humu ulimwenguni ni maandalizi ya Maisha haya ya milele.

Kufuatia hili,,,hiyo ndio maana yetu muhimu kwenye kipindi hiki kukabiliana na swali hili, ya kwamba ***<u>je! ni nani atakaye ingia enda mbinguni?</u>***

Katika Waraka huu wa Paulo kwa Waefeso 5:1-7,,,Mtume huyu aliwaelezea vizuri tena zaidi Waumini kuyahusu maisha baada ya kifo kwa makini sana.

……

1. Basi iweni wafuasi wa Mungu, kama watoto wapenzi;

2. mkaenende katika upendo, kama Kristo naye alivyotupenda, akajitoa kwa ajili yetu kuwa sadaka na dhabihu kwa Mungu kuwa harufu ya kupendeza.

3. Lakini uasherati usitajwe kamwe miongoni mwao, wala uchafu wote wa kutamani;

ninyi, kama iwapasavyo watakatifu;

4. Wala aibu, wala maneno ya upumbavu, wala mizaha, ambayo hayapendezi;

kutoa shukrani.

5. Maana neno hili mnalijua, ya kwamba hakuna mwasherati, wala mchafu, wala mchoyo;

mwabudu sanamu, ana urithi wo wote katika Ufalme wa Kristo na wa Mungu.

6. Mtu awaye yote asiwadanganye kwa maneno yasiyo na maana; ya Mungu juu ya watoto wa uasi.

7. Basi msiwe washiriki wao.

Rafiki yangu,,tunapoisoma Mistari hii,,,tunaziona vizuri sana ***<u>sifa</u>*** za milele za watakaoingia mbinguni.

Tunamwoona Mtume huyu akiwa anayaanza maandiko haya kwa kusema,,“Basi iweni ninyi

wafuasi wa Mungu, kama watoto wapendwa.”

Jambo la kwanza kabisa hapa,,,Mtume anamaanisha ya kwamba sisi kama Wakristo,,ni ***lazima tuwe watu ambao ni waadilifu katika Imani.***

Rafiki yangu,,,imani hii bila shaka ni katika Mwenyezi Mungu.

Anasema,,, Watakuwa wanyoofu katika imani hiyo. Mtume Paulo anaendelea na wazo lingine katika mstari wa pili, “na kuenenda katika upendo kama Kristo naye alivyotupenda sisi.” Hapa alimaanisha ya kwamba,,,Wale waendao mbinguni watakuwa wanyofu kufuata kielelezo cha

Yesu. Watu hawa wanapaswa kuteseka na licha ya hayo watembea katika upendo kama vile Mtume Paulo anavyotuagiza hapa.

Yesu Alifanyika kuwa dhabihu ya Mungu kwetu ile tukaweze kumrudia.

Katika aya ya 2 Mtume anasema,,,“Na amejitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya kupendeza.”

Dada yangu,,Dhabihu hiyo ya Yesu Kristo pale msalabani kwa kweli ndiyo dhabihu pekee inayowezakuturejesha kwa Mungu.

……

Jambo la pili ambalo Mtume huyu anatuambia ni kwamba,,,Mtu atakaye ingia Mbinguni ni ***lazima Ajitengwe na uovu .***

Ndugu yangu,,katika aya ya 3 tunamwoona Mtume Paulo akiwa anaorodhesha semi kadhaa tofauti za mienendo ambayo ni miovu,,,yaani ,, uasherati, uchafu wote, kutamani. Kisha anasema, "Lisitajwe jina kati yenu hata mara moja."

Haya yote msikilizaji wangu ni mambo ambayo yanahusiana na mwiingiliano wa kijinzia katika jamii iwayo yote.

Uchafu, maneno ya kipumbavu na mzaha ni mawazo zaidi katika mstari wa 4. Hizo ni dhambi za usemi ambazo hazipaswi kutajwa.Hii ina maanisha ya kwamba,,, ndimi zetu ni lazima zitakaswe.

Ndugu yangu,,tunapo yasoma maandiko haya,,tuna pata fahamu ya kwamba,,Watu waovu hawana nafasi mbinguni hata kidogo.

Mfano watu kama hao ni pamoja na; wazinzi ambao mienendo yao sio ya kuridhisha.

Dada yangu kwa wale ambao tunataka kwenda mbinguni,,ni lazima tujitenge maovu maana waovu hawatapata nafasi ya kwenda Mbinguni hata kidogo.

……

Jambo la tatu na la mwisho ni kwamba,,atakae kuingia mbinguni ni ***lazima awe imara maishani.***

Hapa Mtume Paulo anatutahadharisha kulihusu swala la udanganyifu maana ndio mwanya wa shetani kutushambulia.

Kufuatia maandiko,,tunaelewa ya kwamba wazazi wetu wa kwanza yaani Adamu na Hawa ,,Bustanini mwa Edeni walimtenda Mungu dhambi baada ya kudanganywa na shetani.

Rafiki yangu,, hadi wa sasa shetani huyo bado anawadanganya kila siku.

Mtume Paulo anatuonya tuwe waangalifu ili mtu yeyote asitudanganye kwa maneno yasiyo na maana.Maanake ni lazima tuwe imara katika maisha.

Sehemu ya mwisho ya mstari wa 6 inasema,,“kwa maana kwa sababu ya mambo haya ghadhabu ya Mungu huja juu ya wana wa kuasi.”

Ndugu yangu,, je!Unaona? Matendo kama haya yanahitaji hukumu ya Mungu na ni lazima Mungu atawaadhibu kwa haki watenda maovu kama hao.

Mtume anasema basi, “msiwe washiriki pamoja nao.”

Rafiki yangu,,Kutokana na mafundisho ya Mtume Paulo, tunajifunza kuhusu wale watakao ingia Mbinguni,,,ambao ni wale watu ambao ni waaminifu, watu waliojitenga na hatimae wale watu ambao ni thabiti.

Kwa neema ya Mungu na huduma ya Roho wake Mtakatifu, wewe Pamoja nami tunaweza kuyatengeneza mapito yetu ili kuingia mbinguni.

OMBI..Mfalme wa Waflme, Baba yetu wa Mbinguni. Ni furaha yetu kujua ya kwamba umetutengenezea njia ya kuingia Mbinguni kwa kuyaacha matendo maovu,,,na kumfuata Yesu Kristo. Tuongoze katika safari hii ya kukufikia .

Ni kwa Yesu tumeombaa…..Amen.....

Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu.Kipindi cha matumaini kutoka Twr ambapo siku hii ya leo tumejifunza kuhusu ni nani atakaye ingia Mbinguni.

Ujumbe umekuwa ni kutoka kwenye Waefeso 5:1-7.

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo shiriki nawe mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Anwani hiyo ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,,ni wimbo Nitaingia Lango naye mtumishi-Mary Wambui

WIMBO…….

Ni kweli kabisa tutakapo ingia Mbinguni,,itakuwa ni furaha tupu. Ni dada yetu Mary Wambui na wimbo nitaingia lango ……..

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505
NAIROBI KENYA x2
Simu/Sms 0721970520 x2
Barua Pepe-barua@twr.co.ke

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara……Kwaheri